# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Juni,2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022**

## RC- KILIMANJARO AIPONGEZA SAME KUFANYA VEMA UKUSANYAJI MAPATO NA USIMAMIZI WA MIRADI



***Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu akizungumza kwenye Baraza Maalum la Madiwani kupitia na kujadili hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) 2022/2023.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepongezwa kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kila mwaka pamoja na usimamizi mzuri wa fedha za Serikali hali iliyosababisha Halmashauri hiyo kupata hati safi toka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kwa miaka minne mfululizo.

Pongezi hizo zimetolewa kwenye kikao Maalum cha Baraza la Madiwani la kupitia hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa fedha za Serikali (CAG) na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu ambapo alisema Same ni muongoni mwa Halmashauri zinazofanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa Miradi.

"Hata kwenye taarifa za Kitaifa Wilaya ya Same imekua ni miongoni mwa Halmashauri ambazo graph yake ya mapato imekua ikipanda kwa zaidi ya miaka minne mfululizo, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Madiwani na watendaji wote wa Halmashauri hii"alisema.

Akizungumza kwenye Kikao hicho Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama alisema Halmashauri inaendelea kujiwekea mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kwamba ukusanyaji mapato unaendelea kuongezeka.

Halmashauri ya Wilaya ya Same imeendelea kufanya vizuri kwenye ukusanyaji mapato ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/21 ilikusanya Bil 2 sawa na asilimia 91.4 ya makisio , mwaka 2021/22 ilikusanya Bil 2.6 (101%) ,mwaka 2022/23 ilikusanya Bil 2.9 (109%) na mwaka Huu 2023/24 Halmashauri imelenga kukusanya Bil 3 ambapo hadi mwezi June 2024 imekusanya Bil 3 (100%).

**SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**
**”Una haki ya kuchagua na kuchaguliwa”**

# “WANANCHI JITOKEZENI MABORESHO YA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA”-DED MHAGAMA



***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Duma,Kata ya Msindo Wilayani Same.***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi wakati wa uboreshaji wa Daftari la kudumu la wapiga kura ambao unatarajia kuanza Septemba 25,2024 hadi Oktoba Mosi 2024 kwenye Mkoa wa Kilimanjaro ikiwemo Wilaya ya Same.

Alisema kuwa kupiga kura ni haki ya msingi kabisa ya kidemokrasia kwa kila raia mwenye sifa ya kupiga kura hivyo ni vyema wananchi wakajitokeza kuhakikisha kuwa wanahakiki taarifa zao ili wawe na sifa ya kupiga kura.

Aidha amehimiza wananchi wenye sifa wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika ngazi za Mtaa na Vijiji ili kuendelea kuimarisha demokrasia hapa nchini.

Nafasi zinazotarajiwa kugombewa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni pamoja na nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji, wenyeviti wa vitongoji na wajumbe wa

Halmashauri ya Kijiji na kwa upande wa Mitaa watakakaochaguliwa ni Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Mtaa.

Wananchi wenye umri kuanzia miaka 18 wanatakiwa kuboresha taarifa zao kwenye Daftari la kudumu la Wapiga Kura wakati wa zoezi hilo ambapo wananchi wenye umri kuanzia miaka 21 na kuendelea wanaweza kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi huo.

## SERIKALI YATOA KIFUTA JASHO CHA TSH.217 MIL. KWA WAHANGA WA WANYAMA WAHARIBIFU

Wizara ya Maliasili na Utalii imetoa kifuta jasho cha Shilingi milioni 217 kwa wahenga wa madhara yatokanayo na wanyama waharibifu kwenye Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro.

Akizungumzia kifuta jasho hicho Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bw. Jimson Mhagama alisema kifuta jasho hicho kimetolewa kwa wahanga 1,515.

"Tunashukuru sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kulipa kifuta jasho kwa wahanga katika Wilaya yetu kwani imesaidia kupunguza malalamiko"alisema Bw. Mhagama.

Kwa upande wake Afisa Wanyamapori Wilaya ya Same, Bw. Thomas Katunzi alisema kifuta jasho kimetolewa kwa familia za watu 06 waliopoteza maisha baada ya kuuliwa na wanyama.

Alisema wahanga wengine waliolipwa ni wahanga wawili waliopata majeruhi baada ya kuathiriwa na wanyama.

"Wengine waliolipwa ni wafugaji ambao mifugo yao 13 iliuawa na wanyama wakali ambapo pia wakulima walilipwa fidia kutokana na mazao yao ekari 2,396"alifafanua Bw. Katunzi

**SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**
**”Una haki ya kuchagua na kuchaguliwa”**

# MBUNGE KILANGO AMSHUKURU RAIS SAMIA KUMPATIA GARI LA WAGONJWA



***Gari la Wagonjwa (ambulance) lililokabidhiwa Kituo cha Afya Myamba***

Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki Mheshimiwa Anne Kilango Malecela amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kukipatia kituo cha Afya Myamba gari la wagonjwa.

Akikabidhi gari hilo Mbunge huyo alisema Mheshimiwa Rais imesaidia kutatua changamoto nyingi za wananchi katika Jimbo lake ambapo pamoja na kuwapatia gari la wagonjwa lakini pia wamejengewa vituo vya Afya vitatu.

"Hili gari ninalolikabidhi hapa leo ni mama Samia ndio amesema lije, kwahiyo naomba mumshukuru mama Samia mara kumi zaidi ya mnavyonishukuru mimi maana bila yeye kuamua hili gari lisingefika hapa"alisema.

Alimshukuru pia Mheshimiwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia Shule mpya ya Msingi ya kisasa ya Anna Kilango na Shule mpya za Sekondari za Misufini na Kalemawe ambapo kwa upande wa kilimo alimshukuru kwa kuwajengea mifereji mikubwa ya umwagiliaji kwenye Kata ya Myamba na Ndungu.

Akitoa shukrani zake kwa Mheshimiwa Rais, mkazi wa Myamba Bw. Daniel Mmbaga alisema gari hilo litakua msaada sana kwa wananchi wa eneo hilo kwani hapo awali wagonjwa walikua wakisafirishwa kwa pikipiki.

"Kumsafirisha mgonjwa kwa pikipiki anapokuwa amezidiwa ni jambo hatari lakini ilikua ndio njia pekee, tunashukuru sana Rais Samia kutupatia, gari hili" alisema.

## SAME YAPOKEA MIL 554 KUTOKA MRADI WA BOOST




***Shule Mpya ya Msingi ya Anne Kilango iliyopo Kata ya Bendera ambayo imejengwa kwa fedha kutoka Mradi wa BOOST***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepokea Shilingi Mil.554.2 kutoka Mradi wa Kuboresha Ujifunzaji na Ufundishaji kwa Shule za Awali na Msingi Tanzania Bara (BOOST) kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Akizungumzia matumizi ya fedha hizo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama alisema fedha hizo zitatumika kujenga matundu 42 ya vyoo na madarasa 15 kwenye shule za Msingi saba.

“Fedha hizi tayari zilishapokelewa kwenye akaunti za shule husika na tayari hatua za awali za ujenzi zimeshaanza, tunatarajia baada ya miezi miwili kuanzia sasa ujenzi huu utakua umekamilika” alisema Bw. Mhagama.

Alizitaja shule zilizonufaika na mgawo huo kuwa ni shule za Mokande,Mferejini na Majevu ambazo kila moja imepata Shilingi milioni 88.6 kwaajili ya ujenzi wa madarasa matatu na matundu sita ya choo, nyingine ni Kirongwe, Karamba na Kizerui ambazo kila moja imepata shilingi milioni 65.6 kwaajili ya ujenzi wa madarasa mawili na matundu suta ya vyoo,na Shule ya Msingi Boda iliyopokea shilingi Milioni 91.6.

Wilaya ya Same pia imepokea fedha Shilingi milioni 96.8 kutoka Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa mazingira Vijijini(Sustainable Rural Water Supply and Sanitation) ambapo fedha hizo zimegawanywa kwenye shule mbili za Mhezi ambayo imepokea shilingi Mil. 48.3 na shule ya Ishinde imepokea milioni 48.5 ambazo zote zitatumika kujenga matundu 17 ya vyoo kwa kila shule.

Nae Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Same Bw.Marclaud Mero alisema mwaka juzi Wilaya ya Same ilipokea kiasi cha shilingi Bil 8 kutoka Mradi wa BOOST fedha ambazo zilitumika kujenga shule mpya mbili za kisasa za Msingi za Kisima na Anna Kilango, pia zilijenga madarasa 39 na matundu ya vyoo.

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutoa fedha za kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye shule za msingi nchini kupitia Miradi mbalimbali ili kusaidia kutatua changamoto mbalimbali za miundombinu.

**SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**
**”Una haki ya kuchagua na kuchaguliwa”**

## RC BABU ARIDHISHWA NA MATUMIZI YA BIL 2 ZA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA SAME




***Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Same Dkt.Charles Msangi (kushoto) akitoa taarifa ya utekelezaji wa Ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ambayo tayari imeshaanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje(OPD) kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdini Babu (mwenye miwani).***

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu ameipongeza Wilaya ya Same kwa Matumizi mazuri ya shilingi bilioni 2 zilizotolewa na Serikali kwaajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya hongera sana kwa usimamizi mzuri, kutumia bilioni mbili kujenga majengo yote haya sio jambo jepesi, niwape hongera sana"alipongeza Mhe.Babu

Fedha hizo zimetumika kujenga majengo nane likiwemo jengo la wagonjwa wa nje, jengo la baba, mama na mtoto, jengo la Utawala, jengo la kuhifadhi Dawa, jengo la kufulia na jengo la mionzi.

Pamoja na fedha hizo pia Wilaya ilipokea milioni 500 kwaajili ya ununuzi wa vifaa tiba hospitalini hapo na tayari vifaa hivyo vimeshanunuliwa na huduma zimeanza kutolewa kwa wagonjwa wa nje (OPD).

## SAME YAPOKEA BIL 3.9 MIRADI YA ELIMU SEKONDARI



***Majengo ya Shule mpya ya Sekondari ya Misufini Goma ambayo imeanza kupokea wanafunzi January 2024.***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Halmashauri hiyo shilingi bil 3.9 kwaajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali kwenye sekta ya Elimu Sekondari kwa mwaka 2023/2024.

Bw. Mhagama alisema kuwa fedha hizo zinatekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa shule za Sekondari Wilayani humo ambapo alisema miradi hiyo ni pamoja na umaliziaji wa Mabweni sita kwenye shule za Sekondari Bangalala, Kwizu, Madiveni, Makanya, Kibacha, Bombo Kimala na ujenzi wa mabweni mawili kwenye shule kongwe ya Sekondari Same na shule mpya ya Misufini Goma.

Alisema Halmashauri pia imepokea fedha kwaajili ya ujenzi wa shule mpya za Sekondari ambazo ni Malindi, Angellah Kairuki, Hedaru, Misufini Goma ambapo shule mbili zimeshapokea wanafunzi na shule mbili zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

"Tumepokea pia fedha za kujenga nyumba tatu za watumishi ambazo ni 2 in 1 kwenye shule za Sekondari Misufuni Goma, Angellah Kairuki, na Malindi na ujenzi wake upo kwenye hatua za awali" alisema Bw. Mhagama

Alisema fedha hizo pia zitatumika kujenga Madarasa mapya 22 na matundu ya vyoo 72 kwenye shule mbalimbali za Sekondari Wilayani humo.

"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha hizi na tunachoweza kumuahidi ni kwamba miradi yote itakuwa na ubora unaotakiwa na itakamilika kwa wakati" alishukuru Mwenyekiti wa Halmashauri ya WIlaya ya Same Mhe.Yusto Mapande wakati akizungumzia mapokezi ya fedha hizo.

**SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**
**"Una haki ya kuchagua na kuchaguliwa"**

# DC MGENI AAGIZA WAKANDARASI KUTOA AJIRA KWA WAZAWA



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni (kushoto) na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mhe.Yusto Mapande (kulia) wakishuhudia utiaji saini wa Mkataba wa kusambaza maji kwenye Vijiji vya Msindo na Mbakweni wenye thamani ya Tsh.Bil.1. Mkataba huo umesainiwa na Meneja wa Ruwasa Abdallah Gendaheka na Kampuni ya BuildTech Engineering Co.Ltd.***

Wananchi wa Vijiji vya Msindo na Mbakweni kwenye Kata ya Msindo wanatarajia kuondokana na adha ya uhaba wa maji baada ya Kampuni ya BuildTech Engineering Co. Ltd kusaini Mkataba wa kusambaza huduma ya maji safi kwenye vijiji hivyo.

Mkataba huo wenye thamani ya shilingi bilioni 1.05 ulisainiwa kati ya Wakala wa Maji na usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Same na Kampuni iliyoshinda zabuni ya Mradi huo ya Build Tech Engineering Co.Ltd.

Akitoa taarifa ya Mradi huo Meneja wa RUWASA Wilaya ya Same Bw. Abdallah Gendaheka alisema Mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Mei 31,2024.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Msindo Mheshimiwa Yusto Mapande aliishukuru Serikali kwa kuwapatia Mradi huo na kuahidi kuusimamia na kuutunza.

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni ameitaka Kampuni ya BuildTech Engineering Co. Ltd kukamilisha Mradi wa Maji wa Msindo-Mbakweni katika muda wa mwaka mmoja kama ulivyo kwenye Mkataba wao na RUWASA.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Bw. Jimson Mhagama alisema wananchi wanachohitaji ni kuona maji bombani hivyo kampuni ya BuildTech Engineering Co. Ltd inapaswa kuhakikisha maji yanapatikana bombani kwa wakati.

## M/KITI MAPANDE ATOA MAELEKEZO KWA MAAFISA TARAFA WAPYA



***Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe.Yusto Mapande akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.***

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mheshimiwa Yusto Mapande amewataka maafisa Tarafa Wilayani humo kuhakikisha wanasimamia vema ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na usimamizi wa Miradi inayotekelezwa katika maeneo yao.

Mwenyekiti alitoa maelekezo hayo kwa maafisa Tarafa wapya walioajiriwa kwenye Wilaya ya Same ambapo alisema kila kiongozi wa Serikali ana wajibu wa kuhakikisha mapato ya Serikali hayapotei na pia Miradi inatekelezwa vema.

"Tunawakaribisha Wilaya ya Same lakini tunawakaribisha zaidi kazini yaani kwenye majukumu ya Serikali, pamoja na kusimamia ulinzi na usalama lakini pia mna wajibu wa kuhakikisha mapato hayapotei kwenye maeneo yenu"alisema Mhe.Mapande.

Maafisa Tarafa wapya ni Robi wa Tarafa ya Gonja, Agape Ndossi wa Tarafa ya Mamba -Vunta, na Jackline Kayega wa Tarafa ya Mwembe-Mbaga

Aidha Mwenyekiti aliwataka watendaji wa Kata kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata chakula cha mchana shuleni.

"Tunatambua kwamba Shule zetu zote zinatoa chakula cha mchana shuleni lakini kuna baadhi ya wazazi bado hawachangii chakula cha watoto wao shuleni, hawa wanaogoma kuchangia wakati uwezo wa kuchangia wanao wahimizwe kuchangia"alisema.

## WANANCHI WA KIJIJI CHA DUMA –MSINDO WAOMBA KUJENGEWA SEKONDARI



***Mzee Harrison Mrutu, Mkazi wa Kijiji cha Duma akiwasilisha ombi kwa Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni kuhusu kujengewa shule mpya ya Sekondari***

Wananchi wa Kijiji cha Duma kwenye Kata ya Msindo Wilayani Same wameiomba Serikali kuwajengea Shule nyingine ya Sekondari kwenye Kata hiyo kwani iliyopo sasa ipo umbali wa zaidi ya kilomita sita toka kilipo Kijiji hicho.

Akizungumza kwenye mkutano uliohudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni, Mkazi wa Duma Bw. Harrison Mrutu aliomba Serikali kuwajengea Shule mpya ya Sekondari kwani Shule ya Kata (Madiveni) wanayoitegemea ipo mbali toka kilipo Kijiji cha Duma.

"Tunaomba Sana tujengewe Sekondari nyingine kwani Sekondari ya Madiveni tunayoitegemea kwasasa ipo mbali Sana ambapo inawalazimu watoto kutembea zaidi ya kilomita 12 kwa siku kwenda na kurudi Shule"alisema Mzee Harrison.

Akijibu maombi hayo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama aliyekuja ameambatana na Mkuu wa Wilaya, aliwataka wananchi hao kuanza kuandaa eneo la ujenzi na kuleta maombi rasmi ambayo yatapitishwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata ili Serikali ione namna bora ya kuwajengea Shule.

Nae Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alisema kwa sasa Serikali inakamilisha Ujenzi wa Bweni kwenye Shule ya Sekondari Madiveni ili Bweni hilo liwe msaada kwa wanafunzi wanaotoka mbali wakati mchakato wa kujenga Shule nyingine ukiendelewa.

**SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**
**”Una haki ya kuchagua na kuchaguliwa”**

# SAME YASOMBA VIKOMBE UMITASHUMTA



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni akiaga Timu ya UMITASHUMTA Wilaya ya Same wakati ikielekea kushiriki Maashindano ngazi ya Mkoa***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amewapongeza washiriki wa mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) kutoka Wilaya ya Same kwa kushinda vikombe sita na kushika nafasi ya tatu ngazi ya Mkoa.

"Tuliitamani sana nafasi ya kwanza lakini hata nafasi mliyoshika sio mbaya ila mwakani ongezeni bidiii"alisema Mhe.Kasilda

Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Same Mwl. Marclaud Mero alisema Wilaya ilijipanga vizuri na lengo likiwa ni kurudi na vikombe vya kutosha katika mashindano hayo.

"Lengo letu halikuwa kushiriki tu mashindano bali lengo lilikua kushinda na kama mnavyoona tumerudi na vikombe vya kutosha kabisa na tumetoka wanafunzi 50 kuunda timu za mkoa"alisema Mwl.Mero.

Naye Mratibu wa UMITASHUMTA Wilaya ya Same Mwl.Nathaniel Msangi alisema vijana wake wamepambana Sana na wamefanikiwa kupata nafasi ya tatu kati ya Halmashauri Saba zilizoshiriki.

"Tupo nafasi nzuri kimkoa lakini lengo letu ni kushika nafasi ya kwanza, mwakani tutapambania nafasi ya kwanza ambayo mwaka huu imechukuliwa na Manispaa ya Moshi ikifuatiwa na Moshi Vijijini"alisema Msangi.

Timu zilizoshinda vikombe kwa kushika nafasi ya kwanza ni Riadha wasichana na wavulana, Mpira wa wavu wavulana na wasichana, Mpira wa kikapu wasichana na wavulana.

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



***Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu akizungumza na wananchi wa Kata ya Ruvu Wilayani Same wakati alipofanya ziara kwenye Wilaya ya Same.***



***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama akitoa ufafanuzi kwa Mkuu wa Mkoa Mhe.Nurdin Babu wakati Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro alipofanya ziara kukagua ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Same.***



***Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same wakifuatilia Kikao cha Baraza la Madiwani, kutoka kushoto ni Jamila Mdee (Diwani V/Maalum), Mathias Mrita (Diwani Kata ya Same) na Yaigongo Mrutu (Diwani Kata ya Ruvu***)



*Mwenyekiti wa Kijiji cha Ruvu Mferejini, Bw. John Mamasita akimvisha vazi la kimaasai Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu kama shukrani kwa kuwatembelea kwenye Kata ya Ruvu.*



*Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni akifurahia jambo na wanafunzi wa Shule ya Msingi Kisima wakati alipofanya ziara shuleni hapo*



*Afisa Afya wa Kata ya Ndungu,Bw.Evans Mangesho akitoa elimu ya afya kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari Misufini Goma*

**SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024**
**"Una haki ya kuchagua na kuchaguliwa"**



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**


**S.L.P 138, SAME**

**Mhariri wa Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Juni, 2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022***